Sheikh, Dr. Falâh Ismâ'îl Mandikâr (hafidhahullâh)

KUHUSU KUMSUSIYA ASIYEFANYA TABDÎ' KWA SHEIKH 'ALÎ HASAN AL-HALABI AL-ATHARÎ NA SUALA LA KITABU 'SWIYÂNAT US-SALAFI' CHA AHMAD BAZMÛL

Huu ni mukhtasar wa tafsiri juu ya ziyara ya nchini Tunisia mnamo: 26th Rabî' ul-Awwal 1434 / sawa na 7th February, 2013 CE na inapatikana hapa:
http://ia600807.us.archive.org/31/items/fala7.halabi.tunis/fala7.halabi.1.mp3

Muulizaji: Sheikh wetu, mimi napendelea kutoa malalamiko yangu kwako kuhusu jambo lililonitokea mimi. Mwanafunzi wa ki-ilimu kutoka nchini Libya alinijia akaninaswihi nihudhurie kikao cha *ma-Salafi*. Aliniswihi nichukuwe msimamo wa *tabdî'* kwa Sheikh al-Halabi na katika kikao hicho pakatokea majadiliano marefu. Mimi nikawa, na naendelea kuwa,na msimamo yakwamba kunatakiwa kubakie kimya kuhusu *tabdî'* yake hiyo. Mimi nikamwambia huyu ndugu: 'Mimi ninaye *Imâm* kuhusiana na kukaa kimya katika suala hili, kwa hakika zaidi ya mmoja'. Nikamtajia hadith ya Mtume (*swallallâhu 'alayhi wasallam): "Yoyote mwenye kumnasibisha Mu'min na jambo asilonalo, basi Allâh atamuandalia makaazi yake Radghat Khabâl mpaka awachane na ayasemayo."* Nikamwambia: 'Mimi simfanyii *tabdî'* juu ya tuhuma na wala sifuati ki-Upofu katika mfano wa mas'ala haya, hususan ikiwa suala lenyewe ni miongoni mwa *fitnah*. Kama niko kwenye usawa, basi nitakuwa nimesalimika kuhusiana na heshima ya Sheikh al-Halabi au mtu mwengine yoyote, na lau kama nitakosea, na ukweli ni kwamba yeye ni *Mubtadi'*, basi utoshelezaji utakuwa umefikiwa kutokamana na maneno ya *ma-Ulamâ'*, vilevile mimi nitakuwa kwenye usalama kwani nawatahadharisha watu dhidi ya kila lenye kuzuliwa au makosa yanayotoka kwake au mtu mwengine yoyote.' Ugomvi ukamalizikia na yeye kuniamuru mimi nikasome kitabu *Swiyânat us-Salafi* cha Sheikh Bâzmul...

Sheikh Falâh Ismâ'îl: (akanikatiza): ... Sheikh gani?!

Muulizaji: Sheikh Ahmad Bâzmul.

Sheikh Falâh Ismâ'îl: Enhe. Hicho kitabu chaitwaje?

Muulizaji: *as-Swiyânah* [kinga]

Sheikh Falâh Ismâ'îl: *as-Swiyânah* [kinga] nini?!

Muulizaji: *as-Swiyânat us-Salafi fiy Radd 'alâ'l-Halabi*.

[Sheikh ‘Abdul-Mâlik ar-Ramadhânî al-Jazâiri (*hafidhahullâh*) amesema: **“Kitabu hiki (cha Ahmad Bâzmul) kimekosolewa na Sheikh ‘Abdulmuhsin al-‘Abbâd!”** Angalia katika http://salafimanhaj.com/pdf/SalafiManhaj JazairiOnStudents. Kitabu hicho vilevile kimekosolewa kwa kina na Abû’l-Abbâs ‘Imâd Târiq bin ‘Abdul’Azîz al-Mukhtâr na Abû Usâmah Yâsîn bin Muhammad Âl-Nazâl katika kitabu chao cha kurasa 375 kiitwacho *al-Ibânah ‘an Khiyânat is-Swiyânah (li Ahmad Bâzmûl) li ‘Adl wa Amânah.* [Ufafaanuzi kuhusu urongo wa kinga (cha Ahmad Bâzmûl) kwa uadilifu na uaminifu]

Sheikh Falâh Ismâ’îl: Hili ndilo jina la hicho kitabu?! Utadhani ni Swiyânah [kinga] ya magari au ni Swiyânah [kinga] ya Ndege?!

Muulizaji: Yeye [huyo ndugu wa ki-Libya] kisha akamuamrisha mtu anichunguze na ahakikishe yakwamba nitafanya hivyo [yaani nikisome hicho kitabu]. Nilipomaliza kukisoma hicho kitabu…

Sheikh Falâh Ismâ’îl: Ajabu hii! Akahakikisha yakwamba amekuwekea mtu akufuatilie ukisome?! Kwanini iwe hivyo?! Kwani yeye alikuwa ni kiongozi kwenye mamlaka au ni vipi?! Ajabu kubwa hii!?

Muulizaji: Nilipomaliza kukisoma kitabu hicho nilipata kutambua mambo fulani ndani yake, na nikaona baadhi ya upendeleo (*Tahâmul*) ndani ya kitabu hicho na nikayajadili haya na baadhi ya ndugu. Kisha haya yalipomfikia mwanafunzi wa ki-ilimu wa ki-Libya, akaamuru yakwamba mimi nisusiwe. Suala hilo likafikiya hadi ya kuzuiwa mimi nisiwaswalishe watu na wakalitilia mkazo hilo, sasa ni ipi naswiha yako kwangu na ndugu wengine?

[Mfano wa upendeleo katika kitabu hicho ni kuhusiana na mas’ala ya madai ya Bâzmûl yakuwa ati Sheikh ‘Ali Hasan anaonelea yakwamba hapana budi ipatikane *ijmâ’* kwa *Jarh* kukubalika, haliyakuwa ukweli ni kwamba Sheikh ‘Ali Hasan alitilia mkazo tu yaliyotangulia kusemwa na *Imâm* adh-Dhahabi, yakwamba ni lazima kupatikane *ijmâ’* kushurutisha *Jarh* juu ya wengine na kuwawajibisha washikamane nayo. Suala hilo limejadiliwa vya kutosha katika kitabu kilichotajwa hapo juu na Abû’l-Abbâs ‘Imâd Târiq na Abû Usâmah Yâsîn bin Muhammad Âl-Nazâl]

Sheikh Falâh Ismâ’îl: Wallâhi, mimi nasema: Kwanza wewe ulifanya makosa kukisoma hicho kitabu alichokupa! Ni bora ungelibaki katika msimamo wako wa kwanza, naam. Wallâhi, kosa ni la kukataliwa, daima. Hapa tunayo Qur’ân, ni kwanini Allâh ametueleza mas’ala ya kufanya makosa? Ili tupate mafunzo. Sio ili Allâh atubainishie makosa ya Mitume, Laa Wallâhi, bali ilikuwa tupate mafunzo. Si sawa yakwamba makosa yahifadhiwe juu yetu, yawapo yametekelezwa na aliyekosea au kutoka kwa wale wenye kumtilia nguvu kwenye makosa, ama kuhusu mimi kutengeneza ‘Bango’ au ‘upanga’ na kufanya *tabdî’*, laa Wallâhi. Sisi hatukuumbwa kwa hili. Wallâhi, unaposoma kitabu miongoni mwa vitabu

vya ki-ilimu, kwa mfano lau utasoma kitabu cha *as-Sunnah* cha *Imâm* Ahmad, *ar-Risâlah* cha *Imâm* ash-Shâfî', Wallâhi itakuwa ni bora kwako wewe kuliko kusoma vitabu vya *Swiyânah* au *Miyânah* au mfano wake!

[Kwa hakika inachosha kuona yakwamba nchini Uingereza (LONDON) kwa mfano, vijana na walioanza kubaleghe, ambao waliokamilisha au kuhitimu kwenye Kitabu cha Madînah - Daraja ya Kwanza (!?) wakiinama na kuinuka ili wajipatie nakala za kurasa 600 za Ahmad Bâzmûl, *as-Swiyânah* wakijitahidi kukisoma na kukifahamu!?]

Wachana na vitabu hivi [yaani, hivyo kama '*As-Swiyânah*' cha Bâzmûl]. Yâ 'Abdullâh, wachana na vitabu hivi, vyote. Ni juu yako kusoma vitabu vya Sunnah, soma vitabu vya Kibâr al-Ulamâ'. Wallâhi sisi hatuna wakati wa kusoma vitu hivi! Sisi hatuna wakati wa vitabu hivyo! Sisi hatukuumbwa kwa ajili hiyo Yâ 'Abdullâh! Ikiwa mtu siku hizi atasoma hivi vitabu vyote vya kukosoana vya mmoja dhidi ya mwengine, basi hatutokuwa na wakati wa kuisoma Qur'ân. Haya yote ni kupoteza wakati na kusababisha migawanyiko miongoni mwa watu. Ndio, twaweza kusema yakwamba 'Ali ana hili na lile, lakini hapana mwana-adamu yoyote isipokuwa anayo makosa, yâ Ikhwân, na 'Ali hapana shaka ni miongoni mwa watu kama hao. Wallâhi kurudi kwake nyuma na kuwacha makosa kunapendekeza mno kwetu kuliko Dunya na vilivyomo ndani yake. Lakini, ama kutuhusu sisi kwenda na kutumia maneno kama hayo basi hili linaongeza tu kututenganisha baina yetu na yeye, na Wallâhi ndugu zangu hii siyo njia ya Waislamu kabisa. Mwanzoni huyu ndugu alitaja maneno mazuri: yakwamba hata kama ni *Mubtadi'*, basi nimebaki salama kwa kutosheka na maneno ya wanavyuoni. Sisi hatuwalinganii watu wasimame nyuma ya 'Ali katika kila suala dogo au kubwa, laa wallâhi, usifanye hivyo. Lakini, vilevile sisi hatufanyi tahkiki kwa ukali. **Subhânallâh, kisha ikatolewa hukmu ya kumsusiya [muulizaji]!? Watawezaje kumzuiya [katika kuwaswalisha watu]?! Ya'nî, Mlibya huyu, akiwa kwao Libya ana uwezo wa kuwazuiya watu wasiswali nyuma ya huyu ndugu hapa [nchini Tunisia]?! "Kumzuiya asiongoze swalâh"?! Utadhani yeye ni Colonel Gadhâfî katika enzi zake! Hata hakuwahi kufikiriya, Colonel Gadhâfî, katika enzi zake yakwamba anaweza kuwazuiya watu wasiswali nyuma ya mtu aliyeko Tunisia!? Aliweza kufanya hivyo?! Gadhâfî alikuwa akimzuiya *Imâm* wapi? Libya! Atamuuwa pia. Huyu ndugu (wa ki-Libya) alikuwa na uwezo wa aina gani, mpaka aseme: "mfuatilieni" na amuamrishe asome kitabu cha *Swiyânah*? Huu ni mfano inaposemwa Mukhâbarât [wapelelezi wa C.I.D], kisha baadae uamuzi ukaletwa utadhani ni azimio la kifalme!**

Ndugu Muulizaji anataka kukatiza...

Sheikh Falâh Ismâ'îl: Laa, laa, wachana naye na usitishike naye wala vitisho vyake! Mwambie: Kitabu hiki chakurudia wewe mwenyewe, sisi hatuna wakati nacho! Bâzmûl huyu amenikosoa mimi, amesema yakwamba amenikosoa mimi na mimi hata sijui yakwamba imefikiya idadi nisiyoijua! Lakini hivi leo imenifikiya mimi yakwamba: "ukosoaji juu yako umefika nambari 5'. Mtu mmoja amenitumia ujumbe usemao: 'akh

Bâzmûl anatarajia yakwamba utayasoma majibu yake kwako, yakwamba utafute sehemu ya faragha na uisome jawabu yake ya tano kwako'!? Nikamwambia yule ndugu: 'Jawabu ya tano?' Mimi hata ya kwanza yenyewe sijaisoma! Naam, Wallâhi mimi sijawahi hata kuisoma ya kwanza, na hata kama itafika jawabu ya 50, msimamo wangu ni kwamba sitozisoma!' Sisi hatuna wakati wa kujitweka nafsi zetu na haya, wallâhi hatuna wakati. Wewe unao wakati wa hayo?! Tumia wakati kwa Dini ya Allâh yâ Sheikh, katika vitabu vya wanavyuoni, wallâhi hilo ni bora kwako wewe. Ingelikuwa ni bora lau kama hungelisoma kitabu hicho, lakini ushakisoma! Lau ningelikuwa na wakati, ningelikutajia maneno ya Ibn Taymiyyah, ambapo alisema yakwamba katika zama za Yazîd, watu walikuwa wakifanyiana mitihani kumuhusu yeye, na katika zama za Hajjâj, watu walikuwa wakifanyiana mitihani kumuhusu yeye: "Wasemaje kumuhusu Yazîd, aliye Fâsiq?" watu walikuwa wakisema na "Wasemaje kumuhusu Hajjâj?" Sheikh ul-Islâm aliyakosoa mas'ala yote haya, wallâhi. Yâ 'Abdullâh, hairuhusiwi kuwafanyia watu mtihani isipokuwa kwa mas'ala matatu:

- ✓ Qur'ân, na msimamo wako kuhusiana na Qur'ân
- ✓ Sunnah, na msimamo wako kuhusiana na Sunnah
- ✓ Maswahaba

Huu ndio msingi kuhusiana na kuwatahini watu, huu ndio msingi kuhusiana na utwi'ifu na ukanushaji. Naam, makosa ya yoyote yakidhihiri waziwazi tunayakwepa na hatufuati katika makosa. Uzushi wa yoyote ukidhihirika waziwazi tunakwepa tena zaidi. Ukafiri wa yoyote ukidhihiri waziwazi, twajikata kutokana naye. Sisi hatumfuatilizii, hatumchunguzi na wala hatumpelelezi yoyote, na hatuyasomi mas'ala haya kabisa yaliyoeneya miongoni mwa wanavyuoni wa sasa.

[Sheikh Abû 'Abdul-Mu'izz Muhammad 'Ali Ferkous al-Jazâirî (*hafidhahullâh*) ametufahamisha yakwamba hii ni kutoka katika utaalamu wa *Jarh wa't-Ta'dîl*, inasitiriwa kwa urahisi na wengine, yakwamba

كلام الاقران يطوى ولا يروى

"Maneno ya wanavyuoni wa sasa yanayohusiyana baina yao huwekwa kando na wala hayatajwi" [*Imâm* adh-Dhahabi amesema katika *Siyâr A'lâm un-Nubalâ',* Vol 7 Uk. 40-41:

Sisi hatudai yakwamba *ma-Imâm* wa *Jarh wa't-Ta'dîl* wamehifadhiwa na makosa na wamelindwa na kufanya makosa kwa mara chache, wala wao hawakuhifadhiwa na kuzungumza na watu walio na uadui na uhasama nao kwa ukali. Kwani inajulikana yakwamba maneno mengi ya wanavyuoni wa sasa wanaposhambuliana huwa hayazingatiwi. Kila ikizidi kupatikana hali ya mtu anapozingatiwa na kukubaliwa na kundi (la wanavyuoni) walio waadilifu katika mazungumzo yao.

Vilevile adh-Dhahabi (*rahimahullâh*) amesema katika Mîzân ul-'I'tidâl, Vol.1; Uk.111:

Wanaposhambuliana wanavyuoni wa sasa, hayo hayafai kuzingatiwa hususan ikiwa imedhihirika kwako yakwamba kuna uhasama baina yao au uzalendo wa madh-hab umeingia au wivu wa mmoja juu ya mwenzake, na hapana aliyesalimika na haya isipokuwa aliyelindwa na Allâh. Mimi sijui kuhusu zama zozote ambazo watu walikuwa hawana matatizo haya isipokuwa waliokuwa katika zama za Mitume na wakweli, na kama ningelitaka ningelitaja vitabu juu ya haya.

Ibn 'Abdul-Barr (*rahimahullâh*) amesema katika Jâmi' ul-Bayân ul-'ilm wa Fadhlihi, Vol.2, Uk.152:

Yoyote mwenye kuaminiwa kuwa ni mwenye kuswadikika, amethibitishwa kuwa yuko salama kuhusiana na 'ilmu na kuswadikika kwake na kuhusika na 'ilmu ni jambo la wazi – basi hapo maneno ya mtu yoyote kumuhusu yeye hayafai kupewa uzito wowote isipokuwa atakapokuja na dalili za wazi na haki katika Jarh yake yenye kuthibitisha Jarh yake kwa kupitia viapo vyenye kufuatiliwa na dalili zenye kuthibitishwa.

http://salafimanhaj.com/pdf/SalafiManhaj JarhWaTadeel.pdf

Kila sifa njema ni yenye kumthubutukia Allâh, sisi tuna wanavyuoni wakubwa kwahivyo tunachukuwa kutoka kwao na tunarejea kwao wao kuhusiana na mas'ala ya dini yetu, ambayo hatuyafahamu vya kutosha au kujua kutoka katika Kitabu, Sunnah au Maswahaba, sisi twaregea kwa Kibâr al-'Ulamâ'. Wachana na huyu, Zayd huyu au 'Ubayd huyu. Twamuomba Allâh atupe sisi na nyinyi afya njema! **Wale wenye Shiddah hii, utawakuta na makuffâr, fussâq na wenye kuabudu makaburi wakiwa wazuri kwao na wanyenyekevu... wallâhi wakenda kwa watu ma'asi, bali makuffâr, Ahlul Bid'ah na wenye kuabudu makaburi, Mâshallâh, ni upole wa aina gani huu, na ukarimu na unyenyekevu hapa?!** Mambo si namna hii Yâ 'Abdullâh, huku ni kuzingatia kusikoaminika kuwa ni ufahamu wa sawa wa Al-Walâ' wal-Barâ', hili linapingana na Al-Walâ' wal-Barâ', Na'am.

Ndugu Muulizaji anataka kukatiza kwa kutaka kuleta wazo la 'Kibâr':

Sheikh Falâh Ismâ'îl: Katika niliyo nayo mimi, naweza kuyakataa maneno ya Kibâr kwa maneno ya Kibâr mwengine. Kwani wewe huna Kibâr [katika msimamo wako]? Wewe unao Kibâr wengi katika msimamo wako! Vilevile mimi najuwa, wallâhi, yakwamba wao hawana maneno yoyote ya Kibâr pamoja nao, wallâhi hawana yoyote! Wana ukosefu wa ufahamu kuhusu Kibâr ul-'Ulamâ', wao humwita mtu yoyote wamtakae 'Kibâr'!

Wallâhi ndugu zangu, ni makosa sisi kujishughulisha na nyakati zetu na ndugu yetu 'Ali al-Halabi au mwengine yoyote, wacheni mambo hayo Yâ Sheikh. Wachana nayo na useme: Mimi nenda zangu kuisoma Qur'ân na Sunnah...